



Viwango vya Kilimohai Afrika Mashariki Uzalishaji wa Viumbe Maji



*Imeandaliwa na Shirika la Kilimohai Tanzania- TOAM,
2026*



In cooperation with



1. Eneo na kipindi cha mpito: EAOPS Sehemu ya 11.1

Shamba la viumbe maji linapaswa kuwa vipi?

- Shamba liwe safi na mbali na uchafuzi wa mazingira.
- Tumia samaki wa asili wasiobadilishwa vinasaba (non-GMO na wape mazingira safi na salama
- Kipindi cha mpito ni kati ya miezi 6-24 kutegemea mfumo wa uzalishaji



2. Mazingira bora na yenye afya:

EAOPS Sehemu ya 11.2


- Mazingira yanapaswa kukidhi mahitaji ya asili ya samaki kama vile afasi ya kutosha, mwang, oksijeni na joto sahihi
- Maji yanapaswa kuwa safi
- Mabwawa yawe na sakafu ya asili inapowezekana
- Msongamano mkubwa wa samaki hautakiwi
- Matanki ya saruji hayashauriwi kutumika.

3. Lishe: EAOPS Sehemu ya 11.6

- Lisha samaki chakula cha kilimohai kitokanacho na mimea na amaki waliovuliwa kwa njia endelevu
- Epuka matumizi ya kemikali na vichochezi vya homoni
- Chakula kisicho cha kilimohai kinaweza kutumika kwa ruhusa maalum na kisizidi asilimia 30



4. Mfumo rafiki kwa mazingira: EAOPS Sehemu ya 11.3



- Mfumo wa kutumia maji yale yale (recirculation) unaruhusiwa kwenye sehemu ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki tu.
- Samaki waliotoroka wakamatwe na taarifa itolewe

5. Afya na Ustawi wa Samaki: EAOPS Sehemu ya 11.7

- Zuia magonjwa kwa kuzingatia Maji safi, usafi wa shughuli zote za eneo husika na kupunguza msongo kwa samaki
- Tumia tiba za asili au mitishamba inapowezekana
- Antibiotics zitumike tu pale inapolazimu sana kwa kufuata masharti maalum
- Vichocheo vya ukuaji na dawa za kinga zisizo lazima hairuhusiwi



6. Usafirishaji na Uvunaji: EAOPS Sehemu ya 11.8

- Washughulikie samaki kwa upole ili kupunguza msongo
- Hakikisha maji ni safi wakati wa usafirishaji na yana oksijeni ya kutosha
- Samaki wapewe ganzi kwanza kabla ya kuchinjwa ili kupunguza maumivu

7. Mimea ya Majini (Mwani na Algae) EAOPS Sehemu ya 11.4

- Mimea ya majini ilimwe au kuvunwa kwa njia endelevu bila kuharibu mazingira
- Maeneo ya uzalishaji yasiwe na kemikali au uchafuzi
- Tumia virutubisho vya asili au vya kilimohai pekee



- Ufugaji wa samaki usiongeze uchafu au virutubisho vingi kwenye maji yanayotoka kwenda mazingira
- Usafishaji wa vifaa ufanywe kwa njia za kifizikia/kawaida kwa kutumia njia za asili.
- Uvunaji usiharibu mazingira ya majini au bioanuwai

Kuhusu kipeperushi hiki

Kipeperushi hiki kinaonesha mahitaji ya msingi ya viwango vya bidhaa za kilimohai vya Afrika Mashariki vijulikanavyo kama East Africa Organic Products Standards (EAOPS). Kiwango hiki kilipitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007 na kufanyiwa maboresho kila baada ya miaka mitano hivyo kuwa kiwango rasmi kwa Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Kipeperushi hiki rahisi kimeandaliwa na Mwamvuli wa Kilimohai Tanzania (Tanzania Organic Agriculture Movement -TOAM) kupitia Mradi wa Kitovu cha Maarifa ya Kilimo Ikolojia Hai Afrika Mashariki (Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology in East Africa – KHEA).

Mradi huu unalenga kuandaa, usambazaji wa maarifa na matumizi ya kilimo Ikolojia hai katika Afrika Mashariki. Unafadhiliwa na GIZ kupitia Biovision African Trust (BvAT)

Unaweza kupata maarifa kama haya na mengine mengi kutoka Tanzania na afrika kwa ujumla kwa kutembelea tovuti: <https://khea-africa.org/> na <https://kcoa-africa.org/>
KHEA Website

Mawasiliano

 info@kilimohai.org

 +255 744 134 999

Machapisho mengine katika mfululizo huu

- Uzalishaji wa Mazao
- Uzalishaji wa Mifugo
- Uchakataji wa Bidhaa za kilimohai
- Ufugaji wa Nyuki